



Taarifa kwa Vyombo vya Habari

16 Julai 2015

Wazazi wengi wanataka watoto wao wafundishwe kwa lugha ya Kiingereza

Wazazi 9 kati ya 10 wanakiri kuwa ya kubadilishwa kwa lugha ya kufundishia kunawaletea watoto matatizo

Tarehe 16 Julai 2015, Dar es Salaam: Wazazi sita kati ya kumi (63%) wanataka watoto wao wafundishwe kwa lugha ya Kiingereza katika shule za msingi na sekondari. Hii ni changamoto kwa watunga sera kwani wazazi 9 kati ya 10 (89%) wanasesma watoto wao wanapata shida zinazosababishwa na kubadilika kwa lugha ya kufundishia wanapotoka shule ya msingi kwenda sekondari.

Maoni haya yametolewa na Twaweza katika utafiti wenyewe kichwa cha habari *Ufunguo wa Maisha?* *Mawazo ya wananchi juu ya elimu*. Muhtasari huu unatokana na *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza barani Afrika kwa njia ya simu mkononi wenyewe uwakilishi wa kitaifa. Maoni haya yanatokana na takwimu zilizokusanywa kutoka kwa wahojiva 1, 381 kutoka Tanzania Bara (Zanzibar haikuhusishwa katika utafiti huu) mwezi Novemba 2014. Takwimu hizi zimekusanya kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambayo iliona umuhimu wa mrejesho kutoka kwa wananchi kuhusu Sera mpya ya Elimu na Mafunzo(2014).

Takwimu hizi zinaonyesha kwamba kuna ongezeko la fursa za elimu. Mwananchi mmoja kati ya kumi (11%) amehitimu elimu ya sekondari ya kidato cha 4. Pia mwananchi mmoja kati ya wanne ana mtoto anayesoma shule ya sekondari. Hii ina maana kwamba vijana wengi zaidi wanazo fursa za kupata elimu ya sekondari.

Licha ya hilo, juhudhi zisiishie kwenye kuenda shule tu. Watoto wanahitaji kupata elimu bora ili shule iwe na thamani kwao. Iwapo watoto hawatajifunza stadi zozote wakiwa shulen, swali muhimu litakuwa kwa nini waende? Pamoja na hayo, matarajio ya wazazi pia ni madogo: nusu yao (49%) wanadhani uwezo wa kusoma na kuandika ndiyo stadi muhimu kwa mwanafunzi anayehitimu kidato cha 4. Tarajio kama hili ni dogo sana kutoka kwa mzazi.

Ila kwa upande mwengine, matarajio ya baadaye ya wazazi kwa watoto wao ni makubwa: wazazi watatu kati ya kumi wangependa watoto wao wawe madaktari (29%) au wawe waalimu (27%).

Kwa jumla wazazi wengi wanaamini kwamba shule za msingi zinawaandaa vema watoto kuijunga na elimu ya sekondari; wazazi sita kati ya kumi (62%) wakiamini hivyo.

"Tunafarijika kuona nafasi iliyotolewa kwa jamii kushiriki katika utekelezaji wa Sera mpya ya Elimu na Mafunzo," alisema Aida Eyakuze Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza. *"Takwimu zetu zinaonyesha kuwa matarajio ya wazazi ni madogo tu na tunajua kwamba hiyo ndiyo sababu mojawapo inayofanya matokeo yawe hafifu. Wanahisa wa rasilimali ya kijamii wasipotarajia matokeo mazuri, hakuna atakayekuwa na ari au motisha ya kuleta mabadiliko. Hivyo ni muhimu sana, kuzihimiza jamii za shule kuchukua fursa iliyotolewa ndani ya sera hii kushiriki katika mjadala wa kitaifa. Tunapaswa kujadili ni mikakati gani itakayotuhakikishia nchi yetu ubora wa elimu. Pamoja na hayo, tunaihimiza Serikali*

kuyachukua maoni haya ya wananchi na kuyatumia katika kuboresha sera mpya na kurekebisha mfumo mzima wa elimu na mafunzo."

---- **Mwisho** ----

Kwa taarifa zaidi:

Risha Chande

Senior Communications Advisor, Twaweza

e: rchande@twaweza.org | t: (+255) (0) 656 657 559

Notes to Editors

Maelezo kwa Wahariri

- Muhtasari huu na takwimu zilizomo zinapatikana hapa www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayomlenga raia na inayokusudia kuleta mabadiliko makubwa Afrika Mashariki. Twaweza inaamaini kuwa mabadiliko ya kudumu hayana budi kuanzia chini kwenda juu. Tumedhamiria kujenga mazingira na kupanua fursa ambazo zitatoa mwanya kwa mamilioni ya watu kuhabarishwa na kuwawezesha kuweza kuleta maendeleo katika jamii zao moja kwa moja na kuifanya serikali iwajibike.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:
Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza_NiSisi